



Jengo la Utumishi,  
Kitalu A, 8 Barabara ya Kivukoni,  
11101 Kivukoni, Dar es Salaam.

0738 246 286 / 0738 246 315

[www.tacaf.go.tz](http://www.tacaf.go.tz)

[mfuko.utamaduni@michezo.go.tz](mailto:mfuko.utamaduni@michezo.go.tz)

[mfukotamadunitz](https://www.facebook.com/mfukotamadunitz)



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

**MFUKO WA UTAMADUNI NA SANAA TANZANIA  
(TACAF)**



**WAOMBAJI WA KIKUNDI**

## UTANGULIZI

Mfuko wa Utamaduni na sanaa umeanzishwa kwa sheria ya ujumuisho wa wadhamini (Trustees' incorporation Act) kama ilivyo rejelewa mwaka 2002 (CAP. 318 R.E.2002) na kupewa hati ya usajili yenye namba 1776 tarehe 30 sepemba, 2020.

## LENGO LA MFUKO

Kuinua ubora wa kazi za utamaduni na sanaa ili ziweze kuijendesha kibashara, kutengeneza ajira nchini pamoja na pato la Taifa.

## SEKTA ZINAZO HUDUMIWA NA MFUKO

- Sanaa za Muziki - Taarabu, Injili, Singeli, Kizazi kipyta, Kaswida, Hiphop, Muziki wa Dansi
- Sanaa za Filamu - Wazalishaji, Waandaaji wa Maudhui, waigizaji, wasambazaji, waongozaji, wapiga picha, waandishi wa miswada, wana mandhali
- Sanaa za Maonesho - Upambaji, Sarakasi, Upishi, Michezo ya Jukwaani, U-DJ, Ushereheshaji, Ngoma za Asili
- Sanaa za Ufundu - Utendengenzaji wa Batiki, Uchoraji, Ususi, uchongaji, Utendengezaji wa Shanga, Ubunifu wa mitindo, Uchoraji wa picha za Tingatinga
- Lugha na Fasihi - Waandishi wa vitabu, wasambazaji, watunzi wa mashairi

## WALENGWA WA MFUKO

- Mtu Binafsi;
- Kikundi; na
- Kampuni

## AINA YA HUDUMA ZA MKOPO

- a) Mikopo ya uendeshaji:  
Kuendesha kazi za walengwa kama vile matamasha, mashindano, kutayarisha au kuzindua kazi za Utamaduni na Sanaa na shughuli zingine zinazofanana na hiso.
- b) Mikopo ya Vifaa  
Kununua vifaa vya kazi vitakavyotumika katika kuzalisha kazi za Utamaduni na Sanaa.
- c) Mikopo ya kujikimu / Dharura  
Mikopo ya muda mfupi kwa ajili ya kujikimu wakati wa safari za kuandaa au kufanikisha kazi za Utamaduni na Sanaa

## VIGEZO VYA WANUFAIKA WA MKOPO KWA WAOMB AJIWA KIKUNDI

- Barua ya maombi ya mkopo ;
- Ujazaji wa Fomu na ambatisho la Andiko la Mradi;
- Muhtasari wa kikao uliosainiwa na wanachama wa kikundi wenye ajenda ya maombi ya maombi ya mkopo;
- Utambulisho wa makazi ya viongozi na eneo la Biashara ya kikundi;
- Picha mbili za viongozi wa Kikundi;
- Kitambulisho cha Taifa/ Hati ya Kusafiria/ Leseni ya Udereva kwa wanakikundi;
- Cheti cha usajili/Utambulisho/Kibali kutoka Taasisi inayomsimamia kazi ya Utamaduni na Sanaa;
- Barua ya utambulisho wa kikundi wa Umoja wowote au Chama kilichosajiliwa kisheria katika Sekta ya Utamaduni na Sanaa na ametambulishwa kwa maandishi na Umoja huo;
- Uthibitisho wa vyanzo vingine vya mapato kama yapo;
- Taarifa ya mauzo ya kazi za Sanaa kuitia Benki Statement au miamala ya simu; na
- Ankra Kifani (endapo mkopo ni wa vitendea kazi/vifaa).

## SIFA ZA MKOPO

- Kiwango cha Mkopo ni kuanzia TZS 200,000/= hadi TZS 100,000,000/=
- Muda wa Marejesho ni miezi 24 (Miaka 2).
- Riba ni asalimia tisa (9%).
- Muda wa rehema (grace period) ni miezi mitatu (3).

## NAMNA YA KUWASILISHA MAOMBI

Maombi yote yatumwe kwa:  
Afisa Mtendaji Mkuu,  
Mfuko wa Utamaduni na Sanaa,  
S.L.P 8031,  
DAR ES SALAAM

Na kuwasilishwa kuitia:  
Barua pepe: mfukoutamaduni@michezo.go.tz